



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA
YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UBORESHAJI WA
DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MWAKA 2024**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Mwaka 2024. Uboreshaji huo utaanza tarehe 01 Julai, 2024 katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora. Ratiba ya mikoa mingine itatangazwa kadri Tume itakavyokuwa inaendelea na zoezi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura 2024 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao katika mfumo wa kusajili watazamaji, asasi za kiraia na vyombo vya habari (Accreditation Management System - AMS) unaopatikana katika anwani ya <https://ams.inec.go.tz>

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe **17 hadi 30 Mei, 2024.**

Taasisi au asasi ya kiraia yenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura inatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

- i. iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- ii. iwe imetuma maombi kupitia mfumo wa Accreditation Management System (AMS) kupitia anwani ya <https://ams.inec.go.tz>
- iii. iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- iv. ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;
- v. katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
- vi. iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
- vii. iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.


Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

- i. kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- ii. kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;
- iii. kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika;
- iv. kujaza anwani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake;
- v. kuainisha vyanzo vya fedha zitakazotumika katika utelekezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura;

- vi. kuambatisha ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika; na
- vii. kuorodhesha katika mfumo watendaji watakaotoa elimu ya mpiga kura walioteuliwa na taasisi au asasi iliyopewa kibali.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Limetolewa leo tarehe 17 Mei, 2024 na:



Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI